JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

# TUME YA UTUMISHI WA UMMA

# USHUGHULIKIAJI WA MASHAURI YA NIDHAMU KATIKA UTUMISHI WA UMMA

**(Mada iliyotolewa kwenye Mkutano Mkuu Jumuishi wa Kitaaluma wa Kwanza wa Mwaka wa Jumuiya ya Maafisa Rasilimaliwatu na Utawala Katika Utumishi wa Umma uliofanyika tarehe 22 - 25 Julai, 2025 Ukumbi wa AICC, Jijini Arusha)**

# YALIYOMO


1.0 Utangulizi
2.0 Mamlaka za Nidhamu katika Utumishi wa Umma
3.0 Mchakato wa nidhamu katika Utumishi wa Umma
4.0 Mashauri ya nidhamu na makosa ya jinai
5.0 Rufaa katika Utumishi wa Umma
6.0 Changamoto katika Ushughulikiaji wa Mashauri ya Nidhamu
7.0 Namna sahihi ya kushughulikia changamoto hizo.
8.0 Hitimisho

## 1.0 UTANGULIZI

Taratibu za ushughulikiaji wa mashauri ya nidhamu katika Utumishi wa Umma zimeainishwa kwenye Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298 (Marejeo ya Mwaka 2025), Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022, Taratibu za Uendeshaji wa Utumishi wa Umma za mwaka 2003; Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009 na Nyaraka na Miongozo mbalimbali inayohusu usimamizi wa Utumishi wa Umma.

## 2.0 MAMLAKA ZA NIDHAMU

Kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298 [Marejeo ya Mwaka 2025] na Kanuni zake za mwaka 2022, madaraka ya kuwachukulia hatua za nidhamu watumishi wa Umma yapo mikononi mwa mamlaka zifuatazo:-

- Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- Katibu Mkuu Kiongozi
- Waziri Mwenye Dhamana na Serikali za Mitaa
- Watendaji Wakuu (Chief Executive Officers)
- Mamlaka za Serikali za Mitaa
- Wakuu wa Idara/Divisheni

## 3.0 MCHAKATO WA MASHAURI YA NIDHAMU

Katika kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya watumishi wa Umma, Mamlaka za Nidhamu zinatakiwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu kama zilivyoainishwa kwenye Mada hii.

## ……Mchakato wa mashauri ya nidhamu

- **Aina za Uendeshaji wa Makosa ya Nidhamu**

Kuna aina kuu mbili za uendeshaji wa makosa ya nidhamu kutegemeana na uzito wa kosa alilolitenda mtumishi. Aina hizo ni :-

**i) Mwenendo wa Makosa Mazito [Kan. 42(1)]**

Mwenendo wa makosa mazito unahusu makosa makubwa ambayo adhabu zake iwapo mtumishi mtuhumiwa atapatikana na hatia, zitasababisha mtumishi:-

## …………Mchakato wa mashauri ya nidhamu

- Kufukuzwa kazi;
- Kushushwa cheo na mshahara; au
- Kukatwa mshahara ghafi kwa asilimia 15 kwa kipindi cha miaka mitatu (3) mfululizo.

NB: Mtumishi ambaye atashushwa cheo na mshahara atahesabika kama amepata cheo kipya ambacho atakitumikia kwa muda uliowekwa kabla ya kufikiriwa kupandishishwa cheo kingine.

## ............Mchakato wa mashauri ya nidhamu

**ii) Mwenendo wa Makosa Mepesi (Kan. 43)**

Mwenendo huu unahusu makosa madogo ambay mtumishi akichukuliwa hatua yanaweza kusababish mtumishi kupewa onyo la maandishi, Karipio a kusimamisha nyongeza ya mwaka ya Mshahara (Kanu ya 43 Sehemu B ya Jedwali la Kwanza).

## ………Mchakato wa mashauri ya nidhamu

Ili haki ionekane inatendeka kabla na wakati wa kushughulikia masuala ya nidhamu, Kifungu cha 25(2)(a)(b) na (c) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298 [Marejeo ya mwaka 2025] lazima kizingatiwe kwa ukamilifu. Kifungu hicho kinasema kuwa, kabla ya kumchukulia hatua za nidhamu mtumishi, lazima masharti ya kisheria yafuatayo yatimizwe:-

## ……Mchakato wa mashauri ya nidhamu

- Mtumishi apewe Hati ya Mashtaka;
- Mtumishi apewe fursa ya kutosha kujitetea;
- Uchunguzi ufanywe kwenye tuhuma husika kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022.

Sehemu ya (V) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022 inafafanua kwa undani taratibu za kuzingatia katika kuendesha mashauri ya nidhamu uwe ni kwa makosa Mazito au Mepesi. Hatua hizo ni kama ifuatavyo:-

## ……Mchakato wa mashauri ya nidhamu

- Kufanya Uchunguzi wa Awali (Kan. 36)
- Kupumzishwa kutekeleza majukumu (Kan. 37)
- Kumsimamisha kazi mtumishi (Kan. 38).
- Hati ya Mashtaka [Kan. 44(1-3)].
  - - Mapokezi ya Hati ya Mashtaka [Kan. 44(5)]
  - - Kurekebisha Mashtaka[ Kan.38(4]
- Kuunda Kamati ya Uchunguzi [Kan. 45(1-3)]
  - - Sifa za Kamati ya Uchunguzi (Kanuni 46).
  - -  Haki za Mtumishi Anayechunguzwa (Kan. 47).
  - - Muda wa kuunda Kamati na kumaliza Uchunguzi [Kan. 47(15 -18)].
  - - Kuhitimishwa kwa Uchunguzi [Kan. 48(1)-(3)].

Utoaji wa Adhabu (Kan.48)

## 4.0 MASHAURI YA NIDHAMU NA MAKOSA YA JINAI

Utaratibu wa kushughulikia mashauri ya nidhamu ambayo pia ni ya jinai umeelezwa chini ya Kan.50(a) – (j), Kan. 51(1)-(4) na Kan. 52. Mtumishi anapokabiliwa na Kesi ya Jinai mambo yafuatayo yatazingatiwa:-

- Mtumishi hatafunguliwa mashtaka ya nidhamu mpaka Kesi ya Jinai iishe Mahakamani [Kan. 50(a)].

- Mashtaka ya nidhamu yakifunguliwa kisha mashtaka ya Jinai yakafunguliwa, mashtaka ya nidhamu yatasimama "stayed" mpaka Mahakama itoe uamuzi [Kan. 50(b)].

## ……….Mashauri ya Nidhamu na makosa ya Jinai

- Akiachiwa huru na Mahakama kwa sababu za kiufundi (on legal technicalities), kuachiwa huko hakutakuwa kizuizi dhidi ya kufunguliwa upya mashtaka ya nidhamu na kuadhibiwa kana kwamba hakukuwa na Shauri la Jinai Mahakamani. [**Kan. 50(c)**].

- Endapo atatiwa hatiani kwa makosa ya jinai itakuwa ni ushahidi wa kuthibitisha kuwa mtumishi husika alitenda makosa ya nidhamu kwa kuzingatia mazingira ya makosa ya jinai aliyotiwa nayo hatiani [**Kan. 50 (i)**].

## ……….Mashauri ya Nidhamu na makosa ya Jinai

- Endapo atapatika na hatia, atahesabika kuwa ametiwa hatiani kwa makosa ya nidhamu kwa kuzingatia ushahidi ule ule uliotumiwa na mahakama [**Kan. 50(e).**

- Mamlaka ya Nidhamu itamzuia kutekeleza majukumu yake (suspension) katika kipindi ambacho itakuwa inashughulikia hatma ya Utumishi wake kwa mujibu wa Kanuni ya 39(1-2). Katika kipindi hiki mtumishi husika hatalipwa mshahara bali atalipwa posho (Alimentary allowance) kwa kiwango kinacholingana na 1/3 ya mshahara kamili alichokuwa analipwa [**Kan. 50(d)**] .

## ……….Mashauri ya Nidhamu na makosa ya Jinai

Kabla ya kutoa uamuzi, Mamlaka ya Nidhamu inatakiwa impatie mtumishi Notisi ya kumtaarifu adhabu inayokusudiwa kutolewa ili mhusika aweze kutoa maelezo yake(mitigation) kuhusu kusudio hilo. **[Kan. 50(f)].**

Shauri la jinai litahesabika kuwa limehitimishwa kama hakutakuwa na rufaa iliyokatwa au baada ya muda uliowekwa wa kukata rufaa kumalizika **(Kan.51(1-2).**

## 5.0 RUFAA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

Kifungu cha 25 cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298, Pamoja na Kanuni ya 60 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022, huanisha Mamlaka za Rufaa katika Utumishi wa Umma kama ifuatavyo:-

(i) Watumishi wa Umma ambao Mamlaka yao ya Nidhamu ni Katibu Mkuu Kiongozi watakata rufaa kwa Rais.

## ……….Rufaa katika utumishi wa umma

(ii) Watumishi wa Umma ambao Mamlaka yao ya Nidhamu ni Waziri mwenye dhamana na Utumishi wa Serikali za Mitaa, Watendaji Wakuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Watumishi ambao Mamlaka yao ya Nidhamu ni Tume ya Utumishi wa Walimu ambao sio Walimu watakata rufaa Tume ya Utumishi wa Umma.

Mtumishi au Mamlaka ya Nidhamu ambayo haitaridhika na Uamuzi wa Tume itakuwa na haki ya kukata rufaa kwa Rais ambaye uamuzi wake utakuwa wa mwisho.

## 6.0 CHANGAMOTO KATIKA USHUGHULIKIAJI WA MASHAURI YA NIDHAMU

Uzoefu ambao umepatikana katika kupitia rufaa za watumishi wa umma zinazowasilishwa Tume ya Utumishi wa Umma kwa mujibu wa Kifungu cha 25(1)(b) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298, umeainisha maeneo yenye changamoto katika kushughulikia mashauri ya nidhamu katika Utumishi wa Umma kama ifuatavyo:-

## ……..Changamoto katika ushughulikiaji wa mashauri ya nidhamu

- **i) Uchunguzi wa Awali**

- Mamlaka ya Nidhamu kutofanya uchunguzi wa awali pale inapolazimika kwa mujibu wa Kan. 36.

- Watumishi watuhumiwa kusimamishwa kazi kupisha uchunguzi badala ya kupumzishwa kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Kan.37(1)

## ……..Changamoto katika ushughulikiaji wa mashauri ya nidhamu

- Watumishi watuhumiwa kupumzishwa kutekeleza majukumu yao kikazi zaidi ya muda uliowekwa kisheria kinyume na Kan. 37(2)(3)(6) na (7).

## ……..Changamoto katika ushughulikiaji wa mashauri ya nidhamu

ii) **Uanzishaji wa Mashauri ya Nidhamu**

- ❖ Hati za Mashtaka kuwa na mashtaka bila maelezo ya mashtaka au kuwa na maelezo ya mashtaka bila mashtaka kinyume na Kan. 44(3) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2022.
- ❖ Kukosewa kwa uandishi wa Hati za Mashtaka mfano maelezo ya shtaka kutofautiana na shtaka kinyume na Kanuni 44(3)
- ❖ Hati za Mashtaka kutotaja Kanuni zilizokiukwa Kan.44(1).
- ❖ Watumishi watuhumiwa  kupewa siku chache za kujitetea baada ya kupewa Hati ya Mashtaka kinyume na Kifungu cha 25(2)(b) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298 kikisomwa kwa pamoja na Kan.44(6)

## …….Changamoto katika ushughulikiaji wa mashauri ya nidhamu

- Watumishi wanaotuhumiwa kutenda makosa ya Kinidhamu kupewa uamuzi wa mashauri yao (adhabu) bila kupewa Hati ya Mashtaka kinyume na Kifungu cha 25(2)(a) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298.

- Hati ya Mashtaka kurudia rudia mashtaka na hivyo mashtaka kuonekana kuwa mengi bila sababu za msingi.

- Tume kupokea Hati za Mashtaka mbili tofauti kwa rufaa moja bila maelezo yoyote kutoka kwa Mamlaka ya Nidhamu.

## ……..Changamoto katika ushughulikiaji wa mashauri ya nidhamu

**iii) Uundaji wa Kamati**

- Kamati za Uchunguzi kutoundwa, kuchelewa kuundwa au kuundwa kinyume na Kifungu 25(1)(2)(c) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298 kikisomwa kwa pamoja na Kan.45(1), 46 na 47(15) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022.
- Baadhi ya Mamlaka za Nidhamu kushindwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 46 wakati wa uteuzi wa Kamati za Uchunguzi ikiwa ni pamoja na;
  - Kuteu wajumbe wa Kamati wasio na sifa
  - Mweyekiti wa Kamati kuteuliwa kutoka ndani ya Taasisi husika

## ……..Changamoto katika ushughulikiaji wa mashauri ya nidhamu

- Baadhi ya Kamati za Uchunguzi kuongezewa muda wa kufanya uchunguzi bila kibali cha Mwenye Mamlaka husika kinyume na Kanuni ya 47(17) na (18) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022.
- Baadhi ya Mamlaka za Nidhamu kutumia Taarifa ya Uchunguzi wa Awali kuthibitisha makosa dhidi ya mtumishi mtuhumiwa badala ya kufanya uchunguzi dhidi ya tuhuma zilizoainishwa kwenye Hati ya Mashtaka.

## ……..Changamoto katika ushughulikiaji wa mashauri ya nidhamu

### iv) Usikilizwaji wa shauri la nidhamu

- Kamati ya Uchunguzi kutomjulisha Mtumishi mtuhumiwa haki zake mbele ya Kamati kwenye barua ya Wito kinyume na Kan.47(5) (7) na (9) ikisomwa kwa pamoja na Aya ya 16.5 ya Taratibu Bora za Uendeshaji wa Masuala ya Nidhamu katika utumishi wa Umma za mwaka 2007.

- Mtumishi mtuhumiwa kutopewa muda wa kutosha kujiandaa na mahojiano na Kamati ya Uchunguzi kinyume na Kanuni ya 47(1)

## ……..Changamoto katika ushughulikiaji wa rufaa mashauri ya nidhamu

- Mwenendo wa Uchunguzi kutoonesha mahojiano ya pande zote mbili na mashahidi husika wakati shauri lilipokuwa linasikilizwa mbele ya Kamati ya Uchunguzi.

- Mtumishi mtuhumiwa kutopewa mwenendo wa Uchunguzi wakati wa mahojiano ili aupitie na kuona iwapo yaliyoandikwa ndiyo yaliyozungumzwa kinyume na Aya ya 25.3.3(c) ya Taratibu Bora za Uendeshaji wa Masuala ya Nidhamu katika Utumishi wa Umma za mwaka 2007.

- Baadhi ya Kamati za Uchunguzi kutowatumia wataalam kutokana na tuhuma zinazochunguzwa pale inapobidi kinyume na Kan.46(6) ya Kanuni za Utumishi wa Umma mwaka 2022.

## ……..Changamoto katika ushughulikiaji wa mashauri ya nidhamu

- Kamati ya Uchunguzi kumhoji Mwajiri na mashahidi wa Mwajiri bila mtumishi mtuhumiwa kuwepo kinyume na Aya ya 16.6 ya Taratibu Bora za Uendeshaji wa Masuala ya Nidhamu katika Utumishi wa Umma za Mwaka 2007.

- Kuendelea kuchunguza shtaka jipya lililobainika wakati wa uchunguzi bila kumjulisha Mamlaka ya Nidhamu ili atoe Hati ya Mashtaka ya nyongeza kinyume na Kanuni 47(13).

- Taarifa ya Kamati ya Uchunguzi kutoonesha iwapo Kamati imethibitisha tuhuma au la

## ……..Changamoto katika ushughulikiaji wa mashauri ya nidhamu

### iv) Utoaji wa Uamuzi wa mashauri ya nidhamu

- ❖ Barua ya uamuzi kuwa na makosa mapya ambayo hayakuwepo kwenye Hati ya Mashtaka.
- ❖ Mamlaka ya Nidhamu kutoa adhabu isiyoendana na makosa yaliyofanywa na mtumishi husika.
- ❖ Barua za Uamuzi kutoeleza haki, mahali na muda wa kukata rufaa kinyume na Kan.61(1)
- ❖ Mtumishi kufukuzwa kazi bila kupewa Hati ya Mashtaka wala kuundiwa Kamati ya Uchunguzi.
- ❖ Mamlaka ya Nidhamu kuchelewa kutoa uamuzi nje ya muda uliowekwa kisheria Kinyume na Kan. 48(6)(9) na (11)

……..Changamoto katika ushughulikiaji wa mashauri ya nidhamu

- Mamlaka ya nidhamu kutoa uamuzi bila kuzingatia Taarifa ya Kamati ya Uchunguzi kinyume na Kan. 48(2) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2022.

- Mamlaka ya Nidhamu kutoa uamuzi unaotofautiana na Mapendekezo ya Kamati ya Uchunguzi bila kueleza Sababu za kutofautiana na mapendekezo hayo kinyume na Kan.48(8).

- Mtumishi mtuhumiwa kuadhibiwa kwa tarehe za nyuma kabla ya kutiwa hatiani kinyume na Kan.48(10).

## ……..Changamoto katika ushughulikiaji wa mashauri ya nidhamu

- Mamlaka za Nidhamu kuendelea na shauri la Nidhamu dhidi ya watumishi wanaokabiliwa na kesi mahakamani kinyume na Kanuni 50(a) na (b).

- Mamlaka za nidhamu kutozingatia hukumu za mahakama katika kutoa uamuzi wa mashauri ya Nidhamu kinyume na Kanuni 50(e), (g), (i) na (j) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022.

## ……..Changamoto katika ushughulikiaji wa mashauri ya nidhamu

**v) Rufaa zinazokatwa Tume ya Utumishi wa Umma**

- Mamlaka za Nidhamu kutowasilisha vielelezo vya Warufani kwa wakati.

- Mamlaka za Nidhamu kuwasilisha vielelezo pungufu kwa Mamlaka ya Rufaa.

- Mamlaka za Nidhamu kuchelewa kutekeleza maagizo ya Tume kwa wakati.

## ……..Changamoto katika ushughulikiaji wa mashauri ya nidhamu

- ❖ Mamlaka ya Nidhamu kutotekeleza au kuchelewa kutekeleza uamuzi/ maagizo ya Mamlaka ya Rufaa kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022

- ❖ Mamlaka za Nidhamu kutochukua hatua za Kinidhamu mapema kwa watumishi ambao ni watoro kazini kwa muda Mrefu.

## 7.0 NAMNA SAHIHI YA KUSHUGHULIKIA CHANGAMOTO ZINAZOJITOKEZA

Katika kukabiliana na changamoto zilizobainishwa, Mamlaka za Nidhamu zinatakiwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuzingatia na kutekeleza ipasavyo matakwa ya Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo iliyopo wakati wa kushughulikia mashauri ya nidhamu kwa watumishi wa umma;

(ii) Kusimamia watumishi wanaoshughulikia masuala ya utawala na rasilimaliwatu ili watekeleze kazi zao na kutoa ushauri kwa umakini mkubwa, uadilifu na kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo iliyopo katika kushughulikia mashauri ya nidhamu kwa watumishi wa umma.

## ………Namna sahihi ya kushughulikia changamoto zinazojitokeza

(iii) Katika mchakato wa mashauri ya nidhamu, Mamlaka za Nidhamu ziwatumie Wanasheria waliopo kwenye Taasisi zao kutoa ushauri na tafsiri ya kisheria;

(iii) Kuwasilisha kwa wakati taarifa na vielelezo vya rufaa vinavyoombwa na Mamlaka za Rufaa ili kuwezesha uamuzi wa rufaa kufanyika katika muda uliowekwa kisheria.

## 8.0 HITIMISHO

Mada hii imeainisha maeneo yenye changamoto katika mchakato wa kushughulikia mashauri ya nidhamu katika Utumishi wa Umma na kuonesha namna ambavyo changamoto hizo zinapaswa kushughulikiwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu wakati wa kushughulikia mashauri ya Nidhamu ya watumishi. Hivyo, mtakuwa mmeongeza uelewa kuhusu namna ya kushughulikia mashauri ya nidhamu katika utumishi wa umma. Uelewa huo utasaidia kuhakikisha mnasimamia nidhamu za watumishi wa Umma ili kuongeza tija kwa Taifa letu.

# ASANTENI